THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# Gredi ya 8

# Mwongozo wa Kutathminia

# SEHEMU A

# SEPTEMBA 2024

Mwongozo huu una kurasa 11 zilizopigwa chapa

© KNEC 2024

# ZOEZI 1:
# KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

## MWONGOZO WA KUTATHMINIA STADI YA KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

## (Mazungumzo ya ana kwa ana na Ufahamu wa Kusikiliza)

| **Kigezo** | **Kuzidi Matarajio**<br><br>**Kiwango 4** | **Kufikia Matarajio**<br><br>**Kiwango 3** | **Kukaribia Matarajio**<br><br>**Kiwango 2** | **Mbali Na Matarajio**<br><br>**Kiwango 1** |
|---|---|---|---|---|
| **Mawasiliano (***matamshi, kiimbo na kusikika***)** | Mwanafunzi anajieleza kwa ufasaha na urahisi, bila makosa ya kimatamshi na anapozungumza anasikika ipasavyo na asemayo yanaeleweka vyema. Maelezo yake yana mantiki na yanafuatilika kwa urahisi. Anazungumza kama mzawa wa lugha hii. | Mwanafunzi anajieleza kwa ufasaha. Ana matamshi yafaayo na kiimbo mwafaka. Ana makosa machache ya kimatamshi na kiimbo lakini anasikika vyema na asemayo yanaeleweka. | Mwanafunzi anajieleza kwa kusitasita. Anafanya makosa ya kimatamshi na kiimbo mara kwa mara na hasisikiki vyema. Maana inaweza kukisiwa kutokana na asemayo. | Ana stadi hafifu za kimatamshi na kiimbo. Anafanya makosa mengi ya kimatamshi. Anakosa mantiki /mfuatano ufaao katika kujieleza. Hasisikiki vyema na asemayo hayaeleweki. |
| **Ufahamu suala lengwa** *(majibu sahihi, matumizi ya msamiati mwafaka*) | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa.<br><br>Anatoa majibu sahihi kwa maswali yote aliyoulizwa kwenye muktadha.<br><br>Anatumia msamiati mbalimbali kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa.<br><br>Anatoa majibu sahihi kwa idadi kubwa ya maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha.<br><br>Anatumia msamiati mwafaka kulingana na muktadha/suala lengwa. | Anatoa maelezo kwa baadhi ya maswali katika muktadha.<br><br>Anatoa majibu kwa baadhi ya maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha.<br><br>Anatumia msamiati mchache kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. | Ana changamoto kuelewa na kutoa maelezo kwa maswali aliyoulizwa kulingana na muktadha. |

| Kigezo | Kuzidi Matarajio<br><br>Kiwango 4 | Kufikia Matarajio<br><br>Kiwango 3 | Kukaribia Matarajio<br><br>Kiwango 2 | Mbali Na Matarajio<br><br>Kiwango 1 |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya ishara za mwili (***jinsi anavyoketi/kusimama, ishara uso, kumtazama mwalimu,ukakamavu)* | Anaketi/ kusimama na kutumia ishara za uso na mwili ipasavyo.<br><br>Anamtazama mwalimu kila wakati kwa nia ya kuwasilisha ujumbe na anazungumza kwa ukakamavu. | Anaketi/ kusimama na kutumia ishara za uso na mwili ipasavyo.<br><br>Anamtazama mwalimu wakati mwingi kwa nia ya kuwasilisha ujumbe na anazungumza kwa ukakamavu. | Anaketi/kusimama na kutumia baadhi ya ishara za uso na mwili.<br><br>Anamtazama mwalimu mara kwa mara na anazungumza kwa kusitasita. Baadhi ya nyakati anazungumza kwa ukakamavu. | Ni nadra sana kutumia ishara za uso na mwili.<br><br>Hamtazami mwalimu kabisa. Anaangalia chini au kando akizungumza. |

**Tanbihi :**

i. Zoezi **I** na Zoezi **II** litathminiwe kwa pamoja ili kukadiria kiwango cha kufaulu cha mwanafunzi.

ii. Zingatia mipaka ya kutuzia katika ukurasa wa **8** na **9.**

iii. Rekodi viwango vya utendaji vya kila mwanafunzi kwa kuzingatia nakala kielelezo katika ukurasa wa **10.**

## ( I) MAZUNGUMZO YA ANA KWA ANA

### Majibu yaliyopendekezwa

1 Mifano ya sehemu za umma ni:

i. Sokoni
ii. Stanini
iii. Maabadini/ sehemu za kuabudia.
iv. Shuleni
v. Mahakamani
vi. Barabarani
vii. Hospitalini

**Tanbihi:**
Hakiki majibu ya mwanafunzi

**Hoja 1 alama 1**

**2 Ushauri kwa wasiozingatia usafi katika sehemu za umma**

a) Mazingira safi yatawaepushia magonjwa.
b) Yatawahakikishia hewa safi.
c) Mazingira yatavutia.
d) Yatahakikisha uhai wa wadudu, ndege na wanyama.
e) Mazingira safi yatatuepushia ajali
f) Yatavutia wawekezaji.
g) Yatawahakikishia mahali salama pa kushiriki michezo na burudani.

**Tanbihi:** ***Hakiki majibu ya wanafunzi***

3 **Mambo atakayozingatia kubadilisha**

a) Kuwashauri wauzaji na wanunuzi kuzingatia usafi.
b) Kuwashauri watu kutupa taka kwenye pipa.
c) Kuhamasisha vijana wenzake kushiriki katika shughuli za kusafisha soko.
d) Kuwafahamisha wahusika umuhimu wa kuwepo kwa majaa ya taka.
e) Kuwazindua/ kuwaelimisha watumiaji wa soko kuhusu madhara yanayoweza kutokana na uchafu.
f) Kuwaomba wazazi / walezi wamsaidia kuwatafuta wadhamini wa kusaidia kuhakikisha usafi katika soko.
g) Kutunga nyimbo/ mashairi ili kuhimiza usafi wa sokoni.

**Tanbihi:** ***Hakiki majibu ya wanafunzi***

4 Taka ikiwa nyingi tutasema ni:

a) Rundo la taka
b) Biwi la taka

**(II): UFAHAMU WA KUSIKILIZA**

5. Ukosefu wa usalama/ Visa vya uhalifu.
6. **Namna uwajibikaji unachangia usalama**.
   i. Hatua mwafaka zitachukuliwa ili kukomesha visa vya uhalifu.
   ii. Itakuwa rahisi kuwatambua wahalifu.

7. **Uhalifu usipokomeshwa yafuatayo yatatendeka:**
   i. Maafa yatatokea.
   ii. Baadhi ya watu watajeruhiwa.
   iii. Uhasama utakithiri miongoni mwa jamii.
   iv. Huenda vita vikazuka.
   v. Mali yataharibiwa.
   vi. Uchumi utadorora.
   vii. Shughuli za elimu zitatatizwa.

   **Tanbihi : Hakiki majibu ya mwanafunzi ipasavyo.**

8. Kushirikiana/ kufanya kazi pamoja.

# ZOEZI 2: KUSOMA KWA SAUTI

## MWONGOZO WA KUTATHMINIA KUSOMA KWA SAUTI

| **Vigezo vya kutathmini** | **Kuzidi matarajio**<br><br>**Kiwango 4** | **Kufikia matarajio**<br><br>**Kiwango 3** | **Kukaribia matarajio**<br><br>**Kiwango 2** | **Mbali na matarajio**<br><br>**Kiwango 1** |
|---|---|---|---|---|
| **Kasi ya usomaji** (*Idadi ya maneno yanayosomwa kwa usahihi kwa muda wa dakika moja*) | Anasoma kwa urahisi na mfululizo wakati wote. Anatumia vituo/ alama za uakifishaji mahali panapofaa wakati wote anaposoma kifungu kuanzia mwanzo hadi mwisho.<br><br>Anasoma kwa usahihi zaidi ya maneno **105** kwa muda wa dakika moja. | Anasoma kwa urahisi na mfululizo. Anatumia vituo/ alama za uakifishaji mahali panapofaa katika kiasi kikubwa cha muda wa kusoma.<br><br>Anasoma kwa usahihi maneno **105** kwa muda wa dakika moja. | Wakati mwingine anasitasita anaposoma. Hazingatii kikamilifu vipumuo na vikomo mwishoni mwa sentensi.<br><br>Anasoma kwa usahihi kati ya maneno **52-104** kwa muda wa dakika moja | Anatatizika kusoma na anarudiarudia maneno mengi na inabidi kurudi nyuma kuanza upya. Anachosoma hakiwezi kufuatilika.<br><br>Anasoma kwa usahihi kati ya maneno 1- 51 kwa muda wa dakika moja. |
| **Kiwango cha sauti na usahihi** (*Kusikika kwa sauti, matamshi na kuunganisha maneno na kuyasoma pamoja kimantiki*) | Anasoma kwa uwazi, ufasaha na kwa sauti inayosikika.<br><br>Anatamka ipasavyo zaidi ya **maneno 105**<br><br>Anaunganisha na kuyasoma maneno pamoja kimantiki wakati wote anaposoma. | Anasoma kwa uwazi na kwa sauti inayosikika.<br><br>Anatamka ipasavyo **maneno yote 105.**<br><br>Anaunganisha maneno mengi na kuyasoma pamoja kimantiki wakati mwingi. | Anasoma baadhi ya sehemu za kifungu kwa uwazi na kwa sauti inayosikika.<br><br>Anatamka ipasavyo kati ya maneno **52-104.**<br><br>Anaunganisha baadhi ya maneno mengi na kuyasoma pamoja kimantiki wakati mwingi | Anasoma neno kwa neno na inabidi asaidiwe. Sauti yake ni chini sana kiasi cha kutosikika..<br><br>Anatamka ipasavyo maneno kati ya **1-51**<br><br>Mara nyingi maneno anayosoma hayaeleweki (anaboboja) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kusoma kwa kutumia ishara** zifaazo. (*Kiimbo, toni na ishara uso)* | Sauti yake ina toni na kiimbo na hubadilika kwa mujibu wa hisia za kifungu.<br><br>Wakati mwingi sauti inabadilika kulingana na wahusika katika kifungu. Anatumia kidatu (ukubwa au udogo) wa sauti wakati wote.<br><br>Wakati wote anatumia ishara za uso ipasavyo anaposoma kifungu. | Sauti yake ina kiimbo.Toni hubadilika kulingana na hisia zinazoibuliwa na kifungu.<br><br>Wakati mwingi sauti inabadilika kulingana na wahusika katika kifungu. Anatumia kidatu (ukubwa au udogo) wa sauti wakati mwingi.<br><br>Wakati mwingi anatumia ishara za uso ipasavyo anaposoma kifungu. | Sauti yake huwa na toni kiimbo wakati mwingine na hubadilika kulingana na baadhi ya hisia za kifungu.<br><br>Habadilishi sauti kulingana na wahusika.<br>Wakati mwingine sauti yake huwa na kiimbo na toni hubadilika.<br><br>Wakati mwingine anatumia ishara za uso ipasavyo anaposoma kifungu. | Sauti yake haibadiliki katika kifungu kizima. Hatumii kiimbo wala toni yake haibadiliki kulingana na hisia za kifungu anaposoma. Habadilishi sauti kulingana na wahusika. Sauti yake inabakia ile ile (sauti bapa)<br><br>Hatumii ishara anaposoma kifungu. |

**MIPAKA YA KUTUZIA SEHEMU (A)**

**KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

| **UPEO/ALAMA (SCOPE)** | **KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)** |
|---|---|
| 4 (Anajibu maswali yote **8** kwa usahihi) | 4 |
| 3 (Anajibu kati ya maswali **6** hadi **7** kwa usahihi) | 3 |
| 2 (Anajibu kati ya maswali **4** hadi **5** kwa usahihi) | 2 |
| 1 (Anajibu chini ya maswali **2** kwa usahihi) | 1 |

**Tanbihi**

Mbali na kigezo cha ufahamu wa suala lengwa, tathmini pia izingatie kigezo cha mawasiliano na matumizi ya ishara za mwili.

**MIPAKA YA KUTUZIA SEHEMU (A)**

**KUSOMA KWA SAUTI (Kasi ya Usomaji)**

| **UPEO/ALAMA (SCOPE)** | **KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)** |
|---|---|
| 4 (Anasoma maneno zaidi ya 10**5** kwa usahihi) | 4 |
| 3 (Anasoma maneno 10**5** kwa usahihi) | 3 |
| 2 (Anasoma kati ya maneno 52-104 kwa usahihi) | 2 |
| 1 (Anasoma kati ya maneno 1-51 kwa usahihi) | 1 |

## MIPAKA YA KUTUZIA SEHEMU (A)

## KUSOMA KWA SAUTI (Mawasiliano, Ufahamu wa Suala lengwa na Matumizi ya Ishara za Mwili)

| **UPEO/ALAMA (SCOPE)** | **KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)** |
|---|---|
| 4 | 4 |
| 3 | 3 |
| 2 | 2 |
| 1 | 1 |

**Tanbihi:**

Tuza alama **4,3,2** na **1** kwa kuzingatia vigezo vilivyotolewa kwenye mwongozo kwa ujumla pasi na kuzingatia kigezo kimoja.

# KISWAHILI GRADE 8 ASSESSMENT SHEET: SEHEMU A

**(Tumia vigezo vya kutathminia ili kurekodi kiwango cha utendaji cha mwanafunzi: 4, 3, 2 ama 1)**

| **NO.** | **JINA LA MWANAFUNZI** | **ZOEZI 1:** **KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** **(Mazungumzo ya ana kwa ana na Ufahamu wa Kusikiliza)** | | | | **IDADI YA MANENO YALIYOSOMWA KWA USAHIHI KWA DAKIKA MOJA** | **ZOEZI 2:** **KUSOMA KWA SAUTI** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 4 | 3 | 2 | 1 | | 4 | 3 | 2 | 1 |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |